"UBORA NA UHAKIKA"

# Sauti ya STAKABADHI

## MIAKA 20 YA WRRB

**MAFANIKIO YANAYOIPA KASI DIRA YA 2050**

**WRRB YAJA NA MIKAKATI MITANO KUKUZA MFUMO WA STAKABADHI**

Yaanza na mifugo
Yavutia uwekezaji wa ghala

soma uk 5



**WAKULIMA WALIPWA**

**TRIL 2.298**

soma uk 6

AJIRA
**31,875**



SAUTI YA STAKABADHI Issue #02 | Agosti 2026

# MIAKA 20 YA WRRB

## MAFANIKIO YANAYOIPA KASI DIRA YA 2050

Kuanzia Julai 1, 2026, Tanzania imeanza rasmi utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kujenga uchumi wa kisasa, shindani na jumuishi unaotegemea uzalishaji wenye tija.

Ili kufikia azma hiyo, sekta ya kilimo inatarajiwa kuwa mhimili mkuu wa ukuaji wa uchumi, huku Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ukiendelea kuwa moja ya nyenzo muhimu za kuongeza thamani ya mazao, kuimarisha masoko na kuongeza kipato cha wakulima.

Mwaka huu pia ni wa kihistoria kwa Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), ambayo imetimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake. Katika kipindi hicho, mfumo umebadili kwa kiwango kikubwa biashara ya mazao nchini kwa kuleta uwazi, ushindani wa bei, malipo kwa wakati na masoko yenye uhakika kwa wakulima.



Tafiti zinaonyesha kuwa wakulima wanaouza mazao nje ya mfumo hupata chini ya asilimia 40 ya thamani ya soko, wakati wanaotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala hupata zaidi ya asilimia 70 ya bei ya soko. Hali hiyo imechangia kuongeza kipato cha wakulima, kuimarisha uchumi wa kaya na kuchochea uzalishaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa WRRB, Asangye Bangu, anasema mafanikio ya mfumo yanaonekana wazi kupitia ongezeko la uzalishaji na mapato ya wakulima.

Anatoa mfano wa zao la ufuta, ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 52,728 mwaka 2021 hadi tani 288,228 mwaka 2025. Katika kipindi hicho, mapato ya wakulima yameongezeka kutoka shilingi bilioni 79 hadi zaidi ya shilingi bilioni 965.

Kwa mujibu wa Bangu, mafanikio hayo yamekwenda sambamba na kuongezeka kwa mapato ya Serikali kutoka shilingi bilioni 9.6 mwaka wa fedha 2020/21 hadi karibu shilingi bilioni 29 mwaka 2024/25.

Anasema katika miaka 20 ya utekelezaji wa mfumo, zaidi ya kilogramu bilioni 5.2 za mazao 18 zimeuzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 11.3. Aidha, mfumo umechangia kuongezeka kwa ajira zaidi ya 30,000 na kupanua shughuli zake katika mikoa 23 nchini.

"Mafanikio haya yanaonesha kuwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala si chombo cha masoko pekee, bali ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi wa Taifa. Uzoefu wa miaka 20 unaonesha kuwa uwekezaji katika masoko yenye uwazi, miundombinu ya kuhifadhi mazao na matumizi ya teknolojia ni msingi wa kuongeza thamani ya kilimo," anasema Bangu.

Anaongeza kuwa WRRB itaendelea kuwa sehemu muhimu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa kuendeleza mfumo unaomnufaisha mkulima, mfanyabiashara na Taifa kwa ujumla.

inaendelea....



# MIAKA 20 YA WRRB

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya miaka 20 ya WRRB yaliyofanyika Mei 19, 2026, Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba, anasema mfumo huo umeondoa vikwazo visivyo vya lazima katika biashara ya mazao, umeongeza uzalishaji kutokana na uhakika wa soko na umeimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Anasema mafanikio hayo yametokana na sera zinazomweka mkulima katikati ya maendeleo, huku kila mdau katika mnyororo wa thamani akipata manufaa yake kwa kuzingatia uwazi, haki na ushindani.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, matumizi ya minada ya kidijitali yameongeza ushindani kwa kuwawezesha wanunuzi wa ndani na nje ya nchi kushiriki kwa wakati mmoja. Alitolea mfano mnada wa kwanza wa ufuta uliofanyika Songwe Mei 9, 2024, ambapo tani 1,144 ziliuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), hatua iliyochangia kupanda kwa bei na kuongeza mapato ya wakulima.

Aidha, anasema ushirikiano kati ya mfumo huo na taasisi za fedha unaendelea kuimarika, huku Serikali ikihamasisha matumizi ya mazao yaliyohifadhiwa kama dhamana ya mikopo ili kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wakulima.

Waziri Mkuu anabainisha kuwa kabla ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, biashara ya mazao ilikabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo wanunuzi wachache, uhaba wa maghala, bei zisizo na ushindani, usalama mdogo wa fedha za wakulima na ukosefu wa takwimu sahihi za uzalishaji.

Anasema mfumo umeleta mageuzi makubwa katika zao la korosho. Kabla ya kuanzishwa kwake, uzalishaji wa korosho katika kipindi cha miaka 20 ulikuwa tani 1,301,935. Baada ya mfumo kuanza kutumika, uzalishaji umeongezeka hadi tani 3,461,850, sawa na ongezeko la asilimia 165.9.




Aidha, mikoa ambayo hapo awali haikujulikana kwa uzalishaji wa korosho, ikiwemo Singida, Tanga, Morogoro, Dodoma, Mbeya, Kigoma, Songwe na Katavi, sasa imejiunga na uzalishaji na kuuza mazao kupitia mfumo huo.

Kwa upande wake, Waziri wa Viwanda na Biashara, Judith Kapinga, anasema Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara kwa kuimarisha ushindani, uwazi na matumizi ya teknolojia katika masoko ya bidhaa.

Anasema mafanikio ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala yametokana na sera sahihi, usimamizi madhubuti na ushirikiano wa wadau mbalimbali, huku akisisitiza kuwa Serikali itaendelea kuimarisha maeneo hayo ili mfumo uendelee kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi, maendeleo ya viwanda na ajira.

Kadiri utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 unavyoanza, mafanikio ya miaka 20 ya WRRB yanathibitisha kuwa uwekezaji katika mifumo ya masoko yenye uwazi, matumizi ya teknolojia na usimamizi bora wa biashara ya mazao ni msingi imara wa kujenga uchumi shindani na endelevu.

Mfumo wa Stakabadhi za Ghala umejidhihirisha kuwa zaidi ya mfumo wa biashara ni nyenzo ya maendeleo inayounganisha maslahi ya mkulima, sekta binafsi na Taifa katika safari ya kuelekea uchumi wa kisasa.

ANNIVERSARY 2006-2026

QUALITY AND ASSURANCE

SAUTI YA STAKABADHI Issue #02 | Agosti 2026

# MIAKA 20 YA WRRB

## PROF. RASHELI: MFUMO WA STAKABADHI NYENZO MUHIMU BIASHARA YA MAZAO

Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Prof. Geraldine Rasheli, amesema Mfumo wa Stakabadhi za Ghala umekuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha biashara ya mazao nchini kwa kuongeza uwazi katika masoko, kuwawezesha wakulima kupata bei zenye tija na kurahisisha upatikanaji wa mikop

Prof. Rasheli akizungumza katika Maadhimisho ya Miaka 20 ya WRRB jijini Dodoma, amesema katika kipindi hicho mfumo huo umeendelea kuwa kiungo muhimu kati ya wakulima, wafanyabiashara, taasisi za fedha na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa mazao.

Amesema kupitia mfumo huo, mazao yanapohifadhiwa katika maghala yanayotambulika, wakulima wanaweza kuyatumia kama dhamana kupata mikopo, huku mauzo yanayofanyika kupitia mfumo yakichangia kuongeza uwazi na ushindani katika masoko

Kwa kipindi cha miaka 20, Mfumo wa Stakabadhi za Ghala umekuwa nyenzo muhimu ya kuimarisha biashara ya mazao, kuongeza uwazi katika masoko, kuwawezesha wakulima kupata bei zenye tija, kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa kutumia mazao yaliyohifadhiwa ghalani, pamoja na kuongeza imani kwa wadau katika mnyororo mzima wa biashara ya mazao," amesema.



Amesema mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho yametokana na maono na usimamizi madhubuti wa Serikali, pamoja na ushirikiano wa wadau mbalimbali, wakiwamo taasisi za fedha, vyama vya ushirika, wawekezaji, wafanyabiashara na wakulima.

"Maadhimisho haya si tu kuonesha tulikotoka, bali ni nafasi ya kutafakari tulipo na kujipanga kwa nguvu mpya kuelekea mfumo imara zaidi, jumuishi na wa kisasa, utakaokwenda sambamba na mabadiliko ya uchumi na mahitaji ya soko la ndani na kimataifa," amesema



SAUTI YA STAKABADHI Issue #02 | Agosti 2026



# GHALA

Mfumo wa stakabadhi za ghala

## WRRB YAJA NA MIKAKATI MITANO YA KUKUZA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imetangaza maeneo matano ya kimkakati itakayoyatekeleza katika kipindi cha miaka mitano ijayo kuanzia mwaka wa fedha 2026/27 hadi 2030/31, yenye lengo la kuimarisha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, kupanua huduma zake na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Bw. Asangye Bangu, ameyasema hayo jijini Dodoma katika mkutano na waandishi wa habari ulioandaliwa na Idara ya Habari – MAELEZO.

Amesema maeneo hayo ya kimkakati ni kupanua mfumo katika sekta mpya za uzalishaji, kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), kuimarisha ushiriki wa taasisi za fedha, kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya maghala na huduma za biashara, pamoja na kuendelea kutoa elimu, kuutangaza na kuukuza Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Bw. Bangu amesema katika mkakati wa kupanua mfumo, WRRB itaanza kuingiza sekta ya mifugo katika Mfumo huo kuanzia mwaka wa fedha 2026/27, ambapo mnada wa kwanza wa mifugo kupitia mfumo huo unatarajiwa kufanyika Wilaya ya Mvomero.

Aidha, amesema bidhaa nyingine zikiwemo mwani, ngozi, mazao ya bustani na bidhaa nyingine zitakazokidhi vigezo zitaendelea kujumuishwa katika mfumo huo.

Amesema WRRB pia itaendelea kuboresha mifumo ya kidijitali ikiwemo WRS-MIS, WRMS na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki ili kuongeza uwazi, ufanisi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wadau wa mfumo.





SAUTI YA STAKABADHI Issue #02 | Agosti 2026



# WAKULIMA

Manufaa ya stakabadhi za ghala

## WAKULIMA WALIPWA TRIL 2.298/- KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

KATIKA 2025/26, Kilo 1,122,246,475 za mazao tisa yenye thamani ya Sh.trilioni 2.679 zimeuzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala (WRS) katika minada ya kidijitali.

Akizungumza jijini Dodoma katika mkutano na waandishi wa habari ulioandaliwa na Idara ya Habari – MAELEZO kuhusu utekelezaji wa shughuli za Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kwa Mwaka 2025/26 na Mwelekeo wa Mwaka 2026/27, Mkurugenzi Mtendaji wa WRRB Bw. Asangye Bangu, amesema kiasi hicho kinajumuisha mazao ya korosho, ufuta, kahawa, kakao, mbaazi, dengu, choroko, soya na chai.

Amesema mauzo hayo yameongezeka kwa asilimia 43.6 ikilinganishwa na kilo 781,659,285 zilizouzwa katika mwaka wa fedha 2024/25, hali inayoonesha kuendelea kuongezeka kwa imani ya wakulima katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na uamuzi wao wa kuuza mazao kupitia mfumo rasmi unaowezesha ushindani wa bei.

Bw. Bangu amesema mafanikio hayo yamewanufaisha wakulima, Serikali na uchumi wa Taifa kwa ujumla, ambapo wakulima walilipwa Sh. trilioni 2.298 kutokana na mauzo ya mazao yao, huku Serikali za Mitaa zikikusanya Sh. bilioni 61.05 kupitia ushuru wa mazao (CESS).



## MKURUGENZI BANGU: AJIRA 31,875 ZIMEZALISHWA KUPITIA WRS

Mfumo wa Stakabadhi za Ghala (WRS) umezalisha ajira 31,875 katika mwaka wa fedha 2025/26 kupitia shughuli mbalimbali za mnyororo wa thamani wa mazao na bidhaa.

Hayo yameelezwa jijini Dodoma na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) Bw. Asangye Bangu katika mkutano na waandishi wa habari ulioandaliwa na Idara ya Habari – MAELEZO wa kutangaza utekelezaji wa shughuli za kwa mwaka wa fedha 2025/26 na mwelekeo wa mwaka 2026/27.

Bw. Bangu, amesema ajira hizo zimetokana na shughuli za ukusanyaji wa mazao na bidhaa, uhifadhi ghalani, upimaji wa ubora, usafirishaji, upakiaji na upakuaji pamoja na huduma nyingine zinazohusiana na biashara kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Aidha, amesema mchango wa WRRB katika kuongeza mapato ya Serikali umeendelea kuimarika, ambapo fedha zilizorejeshwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali zimeongezeka kutoka Sh. milioni 22 mwaka wa fedha 2023/24 hadi kufikia Sh. milioni 140 mwaka 2025/26.

Akizungumzia kuhusu ukaguzi wa bidhaa, Bw. Bangu amesema katika mwaka wa fedha 2025/26, magunia 19,041,651 yenye uzito wa zaidi ya kilo bilioni 1.114 yalikaguliwa katika ghala mbalimbali nchini, hatua iliyochangia kuimarisha uaminifu wa mfumo na kulinda maslahi ya wadau wote wa biashara.



# MFUMO KIDIGITALI

## MHE. CHANDE AIPONGEZA WRRB KWA KUWAWEZESHA WAKULIMA KUFIKIA MASOKO

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Hamad Chande, ameipongeza Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kwa mchango wake katika kuwawezesha wakulima kupata masoko yenye ushindani kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Mhe. Chande ameyasema hayo, baada ya kutembelea banda la WRRB katika Maonesho ya 88 yanayoendelea katika Viwanja vya Dkt. John Malecela, jijini Dodoma.

Amesema WRRB imeendelea kuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha biashara ya mazao kwa kuwawezesha wakulima kupata masoko yenye ushindani, kuongeza thamani ya mazao yao na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.

Aidha, ameipongeza WRRB kwa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na kutoa wito kwa wadau wa sekta ya kilimo kuendelea kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya Maonesho ya Nane Nane ya mwaka 2026 isemayo, "Tambua Soko, Ongeza Tija, Tekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050," kwa kuimarisha mifumo ya masoko, kuongeza tija katika uzalishaji na kuhakikisha wakulima wananufaika na fursa zilizopo katika mnyororo wa thamani wa mazao.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Uratibu Huduma ,Bw. Mwita Thomas ameeleza kuwa WRRB itaendelea kuboresha huduma zake, kuimarisha usimamizi wa mfumo huo kwa kushirikiana na wadau ili kuhakikisha sekta ya kilimo inakuwa chachu ya maendeleo ya uchumi na ustawi wa wananchi.



## WRRB MBIONI KUKAMILISHA MABORESHO YA MFUMO WA KIDIGITALI KUONGEZA UFANISI

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imesema ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha maboresho ya mfumo wake wa kidigitali yatakayoongeza ufanisi katika usimamizi wa shughuli za ghala pamoja na utoaji wa leseni kwa waendesha maghala, wakaguzi na Mameneja Dhamana.

Akizungumza katika Maonesho ya Nanenane yanayoendelea katika Viwanja vya Dkt. John Malecela, Nzuguni jijini Dodoma, Kaimu Mkurugenzi wa Uratibu wa Huduma wa WRRB, Bw. Mwita Thomas, amesema maboresho hayo yanalenga kurahisisha utoaji wa huduma kwa kuufanya mfumo usomane na mifumo mingine muhimu ya Serikali, hatua itakayopunguza muda wa kupata leseni na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma.


Amesema sambamba na maboresho hayo, WRRB inaendelea kutekeleza mikakati ya kupanua matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kuwezesha bidhaa zote kuuzwa kupitia mfumo huo, hatua itakayoongeza masoko, uwazi na ushindani wa biashara nchini.

"Kwa sasa mfumo unafanya kazi katika zaidi ya mikoa 23 kwa bidhaa mbalimbali. Vilevile, Bodi ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uuzaji wa mifugo kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, na zao la mwani nalo litauzwa kupitia mfumo huu," amesema Bw. Mwita.

Ametoa wito kwa wananchi, wakulima, wafugaji, wafanyabiashara na wadau wengine kutembelea banda la WRRB katika Maonesho ya Nanenane ili kupata elimu kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Ghala pamoja na fursa mbalimbali zinazotokana na matumizi yake.

SAUTI YA STAKABADHI
Issue #02 | Agosti 2026

# MAHINDI



## WADAU RUKWA WAKUBALIANA MAHINDI KUUZWA KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

WADAU wa zao la mahindi mkoani Rukwa wamekubaliana kuuza mahindi kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na mnada wa kwanza unatarajiwa kufanyika mwezi Agosti, 2026, ili kuimarisha biashara ya zao hilo, kuongeza uwazi wa soko na kuwawezesha wakulima kupata bei zenye ushindani.

Makubaliano hayo yamefikiwa katika kikao cha wadau kilichoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mhe. Charles Makongoro Nyerere, Julai 28, 2026, kilicholenga kujadili maandalizi ya kuanza kutekeleza mfumo huo kwenye zao la mahindi.

Kikao hicho kimehudhuriwa na wawakilishi wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Wakuu wa Wilaya za Nkasi na Kalambo, viongozi wa vyama vya ushirika, Umoja wa Wafanyabiashara pamoja na wakulima.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, mauzo ya mahindi yatafanyika kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa kutumia Meneja Dhamana, huku minada ikiratibiwa kupitia vyama vya ushirika.

Akizungumza katika kikao hicho, Mhe. Makongoro amewataka wadau wote kushirikiana kuhakikisha mfumo huo unatekelezwa kwa ufanisi ili kuongeza tija kwa wakulima na kuimarisha masoko ya mahindi mkoani humo.





## WRRB, MISRI WAJADILI USHIRIKIANO WA KIBIASHARA KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Mkurugenzi wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Bw. Asangye Bangu, amekutana na kufanya mazungumzo na Afisa Biashara kutoka Ubalozi wa Misri nchini Tanzania, Bw. Wael Aref, kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kibiashara kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kupanua masoko ya mazao na mifugo kati ya nchi hizo mbili.

Mazungumzo hayo yamefanyika jijini Dar es Salaam ambapo Bw. Bangu ameelezea majukumu ya WRRB pamoja na namna Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unavyowawezesha wakulima na wazalishaji kupata masoko yenye ushindani, kuongeza thamani ya mazao yao, na kuunganishwa moja kwa moja na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi.

Amesema mfumo huo umeendelea kuwa nyenzo muhimu katika sekta ya kilimo kwa kuweka mazingira ya uwazi, kuongeza ushindani wa bei, na kuhakikisha wazalishaji wanapata uhakika wa masoko yao.

Aidha, viongozi hao wamejadili pia uwezekano wa kupanua wigo wa ushirikiano huo kwa kuingiza mifugo hai katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kuongeza aina ya bidhaa zinazoweza kuuzwa kupitia mfumo huo na kufungua fursa mpya za biashara kati ya Tanzania na Misri.

# MAFUNZO

## WRRB YAWAJENGEA UWEZO WATENDAJI WA GHALA, MSIMU WA MBAAZI NA DENGU



Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imetoa mafunzo ya utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa msimu wa biashara wa mazao ya mbaazi na dengu 2026/2027, huku ikiwataka watendaji wa ghala kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza mfumo huo.

Akifungua mafunzo hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Uratibu Huduma wa WRRB, Bw. Thomas Mwita, amesema washiriki wanapaswa kuyatumia mafunzo hayo kujijengea uwezo, kufanya kazi kwa weledi na kuzingatia maadili ili kuhakikisha mfumo unaendelea kuwa na ufanisi.

Amesema mafunzo hayo ni sehemu ya jitihada za WRRB kuimarisha utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, kuongeza ufanisi katika biashara ya mazao na kuchochea fursa za ajira kwa vijana, hivyo kuongeza mchango wa sekta za kilimo, viwanda na biashara katika ukuaji wa uchumi.

## SERIKALI YAHIMIZA USIMAMIZI BORA WA GHALA KUINUA BIASHARA YA MAZAO



Watumishi na wasimamizi wa shughuli za ghala nchini wametakiwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, weledi na uwajibikaji ili kuimarisha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kuongeza ufanisi katika biashara ya mazao ya kilimo.

Wito huo umetolewa na Afisa Tawala wa Wilaya ya Morogoro, Bi. Janeth Chatta, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, alipokuwa akifunga mafunzo ya wasimamizi wa shughuli za ghala kwa msimu wa biashara wa mbaazi na dengu 2026/2027 yaliyofanyika wilayani humo

Bi. Chatta amesema uadilifu wa watendaji wa mfumo ni msingi wa kujenga imani kwa wakulima, wanunuzi na taasisi za fedha, huku akisisitiza kuwa Mfumo huo umeendelea kuwa nyenzo muhimu ya kuhakikisha biashara ya mazao inafanyika kwa uwazi, ubora na ushindani.

Amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuhimiza matumizi ya Mfumo huo pamoja na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) ili kuongeza thamani ya mazao, kupanua fursa za masoko yenye ushindani na kuongeza manufaa kwa wakulima.

Aidha, amewataka washiriki kutumia maarifa waliyoyapata kutekeleza majukumu yao kwa weledi, kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kuhakikisha taarifa za mazao zinakuwa sahihi na kwa wakati.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Uratibu na Ubora wa WRRB, Bw. Mwita Thomas, amewataka wahitimu wa mafunzo hayo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu walizofundishwa ili kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, weledi na uwajibikaji, pamoja na kulinda hadhi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na WRRB yamefanyika kwa siku tano na yamehudhuriwa na washiriki 103 kutoka kampuni za uendeshaji wa ghala na wadau mbalimbali wa Mfumo huo.

# WRRB YATUNUKIWA TUZO KWA MCHANGO WAKE KATIKA MABORESHO YA MNYORORO WA THAMANI WA KILIMO

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imetunukiwa tuzo ya kutambua mchango wake katika kufanikisha utafiti kuhusu maboresho ya kisasa ya mnyororo wa thamani wa kilimo uliofanywa na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Maendeleo ya Canada (IDRC-CRDI) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Tuzo hiyo imekabidhiwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa WRRB, Bw. Asangye Bangu, na Meneja wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Bodi hiyo, Bw. Elfaraja Kintingu.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Bw. Bangu amesema heshima hiyo ni uthibitisho wa nafasi muhimu ya WRRB katika kuimarisha sekta ya kilimo kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, ambao umeendelea kuongeza ufanisi wa biashara ya mazao, uwazi wa masoko na ushindani wa bei katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Amesema WRRB itaendelea kushirikiana na taasisi za utafiti na wadau mbalimbali katika kuendeleza ubunifu na maboresho yanayochochea maendeleo ya mnyororo wa thamani wa kilimo kwa manufaa ya wakulima na uchumi wa Taifa.

Awali, akielezea kuhusu tuzo hiyo, Bw. Kintingu amesema imetolewa kwa kutambua ushirikiano na mchango wa WRRB katika kufanikisha utafiti huo, ambapo watafiti walitembelea ghala mbalimbali nchini ili kujionea utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na mchango wake katika kuimarisha biashara ya mazao, kuongeza uwazi wa masoko na kuboresha mnyororo wa thamani wa kilimo.



# WRRB, TMX NA CCWT WAELIMISHA WADAU KUHUSU MINADA YA MIFUGO KIDIGITALI

WAFUGAJI na wafanyabiashara wa mifugo nchini wanatarajiwa kunufaika na minada ya mifugo kidigitali kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, unaolenga kurahisisha upatikanaji wa masoko, kuongeza ushindani na kuboresha ufanisi wa biashara ya mifugo.

Hayo yamesemwa na Afisa Ubora wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Bw. Anatolius Kabyemela, wakati wa utoaji wa elimu kwa wadau na wafanyabiashara wa mifugo katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani. Elimu hiyo imetolewa kwa ushirikiano kati ya WRRB, Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) na Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT).

Bw. Kabyemela amesema mfumo huo utawaunganisha wafugaji na wanunuzi kwa urahisi zaidi, hivyo kuwawezesha wanunuzi kushiriki katika minada na kufanya manunuzi bila kulazimika kusafiri kutafuta mifugo au masoko.

Ameongeza kuwa mfumo huo utatoa fursa kwa wafugaji wenye mashamba makubwa kuyatumia kama maghala ya mifugo, hatua itakayowezesha minada kufanyika katika maeneo hayo kwa ufanisi zaidi na kuwafikia wanunuzi wengi ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wao, wafanyabiashara wa mifugo wamepongeza mpango huo wakisema utarahisisha biashara, kuongeza ushindani na kupanua fursa za masoko

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Bw. Shabani Makia, ameomba kuwepo kwa utaratibu utakaowezesha wafanyabiashara kutumia mfumo huo kuuza mifugo katika masoko ya kimataifa, hatua itakayopanua wigo wa biashara na kuwafikisha kwa wanunuzi kutoka nje ya Tanzania.



# PARACHICHI NA NAZI

## DC MUFINDI NA WRRB WAJADILI UTEKELEZAJI WA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA KWENYE ZAO LA PARACHICHI

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Dkt. Linda P. Salekwa, amekutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Bw. Asangye Bangu, kujadili namna ya kuingiza zao la parachichi katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kuongeza ufanisi wa biashara ya zao hilo na kuwanufaisha wakulima.

Katika kikao hicho kilichofanyika hivi karibuni, viongozi hao wamejadili utaratibu wa kuuza parachichi ikiwa bado shambani ili kulinda ubora wa zao, kupunguza upotevu baada ya mavuno na kuwawezesha wakulima kupata soko lenye ushindani lililo na bei zenye tija.



Aidha, wamesisitiza umuhimu wa kuendelea na tathmini za kitaalamu pamoja na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali ili kuandaa utaratibu utakaowezesha zao la parachichi kuingizwa rasmi kwenye Mfumo huo kwa kuzingatia ubora wa zao, mahitaji ya soko na maslahi ya wakulima.





## HALMASHAURI YA MAFIA YAJIPANGA KUINGIZA ZAO LA NAZI KWENYE MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Halmashauri ya Wilaya ya Mafia imejipanga kuingiza zao la nazi katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa lengo la kuongeza thamani ya zao hilo, kuboresha masoko na kuimarisha kipato cha wakulima.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mhe. Gulam Mohammed, amesema mfumo huo utaleta manufaa makubwa kwa wakulima wa nazi kwa kuwa utaongeza uwazi katika biashara, kupanua fursa za masoko na kuwawezesha kupata bei zenye ushindani na tija.

Ameeleza kuwa Halmashauri itaendelea kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na wadau wengine kuhakikisha maandalizi yote yanakamilika ili wakulima wa zao hilo waanze kunufaika na mfumo huo.

